



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



Dar es Salaam, 15 Julai, 2023

TAARIFA KWA UMMA

KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA UDAHILI KWA WAOMBAJI WA SHAHADA YA KWANZA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU KWA MWAKA WA MASOMO 2023/2024

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Vyuu Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma, Taasisi za Elimu ya Juu na Wadau wote wa Elimu ya juu ndani na nje ya nchi kuwa dirisha la maombi ya udahili kwa waombaji wa Shahada ya Kwanza kwa mwaka wa masomo 2023/2024 limefunguliwa rasmi **kuanzia leo tarehe 15/7/2023**. Dirisha hili litakuwa wazi hadi tarehe **4/8/2023**.

2.0 UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI YA UDAHILI KWA MWAKA WA MASOMO 2023/2024

2.1 Makundi ya Waombaji wa Udahili

Maombi ya Udahili wa kujiunga na Shahada ya Kwanza yanahusu makundi matatu ya waombaji:

- Wenye sifa stahiki za Kidato cha Sita;
- Wenye sifa stahiki za Stashahada (Ordinary Diploma), au sifa linganifu; na
- Wenye sifa stahiki za Cheti cha Awali (Foundation Certificate) cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Ili kufahamu sifa stahiki kwa makundi matatu yaliyotajwa hapo juu, vyuo na programu zilizoruhusiwa kudahili, waombaji wanaelekezwa kusoma vigezo vilivyooneshwa katika vitabu vya mwongozo wa maombi ya Udahili vinavyotolewa na TCU (Undergraduate Admission Guidebooks for 2023/2024) vinavyopatikana katika tovuti ya TCU www.tcu.go.tz.

2.2 Utaratibu wa Kutuma Maombi ya Udahili

- Maombi yatumwe moja kwa moja kwenye vyuo ambavyo muombaji amevichagua na kuchagua programu za masomo anazozipenda.
- Maelekezo mahsusi ya jinsi ya kutuma maombi yanatolewa na vyuo husika.

2.3 **Vigezo na Sifa za Waombaji Udahili**

Vigezo na sifa katika programu mbalimbali za masomo vinapatikana katika tovuti za vyuo husika na katika vitabu vya mwongozo wa maombi ya Udahili (Undergraduate Admission Guidebooks for 2023/2024) vinavyopatikana kwenye tovuti ya TCU www.tcu.go.tz.

2.4 **Masuala Muhimu ya Kuzingatiwa na Waombaji**

- a) Kusoma mwongozo wa udahili uliotolewa na TCU kwa makini na kuelewa kabla ya kuanza kutuma maombi ya udahili;
- b) Kuingia katika tovuti za vyuo ili kujua taratibu za kutuma maombi;
- c) Kutuma maombi moja kwa moja vyuoni kupitia mifumo ya kielektroniki iliyowekwa na vyuo husika;
- d) Kuwasiliana na vyuo moja kwa moja na kupata taarifa za kina kuhusu programu za masomo ili kujiridhisha kabla ya kutuma maombi; na
- e) Waombaji wenye vyeti vilivyotolewa na mabaraza ya mitihani nje ya nchi ni lazima wawasilishe vyeti vyao Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) kwa vyeti vya Elimu ya Sekondari au Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa vyeti vya Stashahada ili kupata ithibati ya ulinganifu wa sifa zao kabla ya kutuma maombi ya udahili.

Tume inawahimiza waombaji wote wa udahili kuendelea kupata taarifa sahihi kupitia tovuti ya TCU www.tcu.go.tz, tovuti za vyuo vilivyoruhusiwa kudahili wanafunzi wa Shahada za Kwanza, pamoja na taarifa mbalimbali zinazotolewa na TCU kupitia vyombo vya habari.

3.0 **TAHADHARI**

Tume inatoa wito kwa waombaji wote wa Shahada ya Kwanza, endapo watahitaji kupata ufafanuzi wa suala lolote linalohusu udahili, wawasiliane moja kwa moja na vyuo husika. Aidha, iwapo watahitaji maelezo ya jumla wanaweza kuwasiliana na TCU kwa kutumia barua pepe es@tcu.go.tz.

Pia, TCU inawaasa wananchi kuepuka kutapeliwa na watu wanaojiita mawakala au washauri wanaodai wanatoa huduma ya jinsi ya kujiunga na vyuo vya elimu ya juu hapa nchini.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa

KATIBU MTENDAJI
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA